JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

TAKUKURU Mkoa,
Mtaa wa Mahakama,
S. L. P 1419,
53103 Mbeya.

Barua pepe: rbombeya@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz
Simu ya Bure : 113

TAARIFA KWA UMMA

Mbeya
Novemba 2023

TAKUKURU MBEYA YASHIRIKISHA WANANCHI KUZUIA VITENDO VYA RUSHWA KWENYE MIRADI YA MAENDELEO YENYE THAMANI YA SH. 37,087,551,581.4

1.0 UTANGULIZI

Ndugu wanahabari,

Leo tumekutana tena katika ofisi yetu ya TAKUKURU Mkoa wa Mbeya ili kupitia ninyi tuweze kuuhabarisha umma kuhusu utendaji kazi wa Ofisi yetu kwa kipindi cha miezi mitatu ya kuanzia **Julai** hadi **Septemba, 2023.**

Kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura 329 toleo la mwaka 2022, TAKUKURU ina majukumu makuu matatu ambayo ni Kuelimisha jamii juu ya rushwa na madhara yake, Kufanya chambuzi za mifumo kwenye Taasisi za umma na binafsi ili kubaini mianya ya rushwa na kushauri namna bora ya kuziba mianya hiyo, pamoja na kufanya uchunguzi wa tuhuma za rushwa na kuwafikisha watuhumiwa mahakamani baada ya kupata kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini.

2.0 SUCCES STORY

Kiasi cha Tsh. 50,000,000/= zaokolewa kutoka katika kikundi cha Isongole Bamboo Group

Isongole Bamboo Group ni kikundi kilichopo katika kata ya Isongole katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ambacho kinajishughulisha na utengenezaji wa bidhaa za Mianzi kama vile vikapu vya kuwekea nguo, mikoba, viti, meza na vinginevyo na biashara ndogo ndogo. Kikundi hiki kimeanza mwaka 2001 na kimesajiliwa mwaka 2017 kwa hati namba RDC/GR.0250/2017.

Kikundi kilikuwa na mashine ambazo zilikuwa na uwezo wa kuchakata bidhaa za mianzi ambazo zimekuwa zikiuzwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Mnamo tarehe 27/12/2021 kikundi kiliomba mkopo na ilipofika tarehe 11/02/2022 kikundi kilipokea fedha Tsh. 50,000,000/= kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwa ajili ya ununuzi wa mashine sita ili kuongeza na kutimiliza mlolongo wa uzalishaji wa vijiti vya kuchokonolea meno (Stick) kulingana na andiko lao la maombi ya mkopo.

Wakati wa utekelezaji wa mradi huo, hali ya ununuzi wa mashine ilionekana kuwa ngumu na hivyo kikundi kuamua kubadili matumizi ya mkopo bila kufuata utaratibu, hali iliyopelekea kushindwa kurejesha mkopo huo kama mkataba unavyoelekeza.

Kutokana na hiyo hali, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe. Juma Homera, kupitia Baraza maalum la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe aliagiza TAKUKURU ifuatilie uhalali wa matumizi ya fedha hizo. Baada ya kufuatailia ilibainika kuwa fedha hizo walizigawana wana kikundi ili kila mtu akazitumie katika biashara zake na kurejesha mkopo kwa wakati waliojipangia na kiasi kidogo cha fedha kiliingizwa katika mradi uliokuwa unaendelea wa kutengeneza bidhaa za mianzi.

TAKUKURU iliingilia kati ambapo ilikaa kikao cha Pamoja na wana kikundi hao na kwa Pamoja ikakubalika kuwa kikundi kianze kurejesha fedha ambazo zilikuwa zimebakia ambazo ni Tsh.43,000,000//=.
Kuanzia Mwezi Julai, 2023 hadi Septemba, 2023, Kikundi hicho tayari kimewasilisha TAKUKURU fedha Tsh. 11,860,000/= na tayari zimeingizwa kwenye akaunti ya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ili vikundi vingine viendelee kunufaika na

mikopo hiyo. Urejeshaji wa fedha hizo bado unaendelea kama makubaliano yalivyofikiwa.

3. UZUIAJI RUSHWA NA UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Katika kipindi hicho, TAKUKURU Mkoa wa Mbeya ilitekeleza kazi za uzuiaji rushwa katika maeneo mawili ambayo ni ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, pamoja na uchambuzi wa mifumo.

3.1 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo

Katika kipindi hicho, Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Mbeya ilifanya ufutiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo **59** yenye thamani ya jumla ya **Shs 33,347,303,359.4** Lengo la kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo ni kuhakikisha kuwa miradi yote inatekelezwa kwa ubora uliokusudiwa na kwa thamani halisi ya fedha iliyotolewa na kutumika, na pia kuhakikisha utekelezaji wa miradi hiyo unakamilika ndani ya muda uliopangwa ili wananchi wapate huduma iliyokusudiwa na Serikali. Aidha, katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi hiyo **61**, jumla ya miradi **3** yenye thamani ya jumla ya **Shs** 1,011,100,000 ilibainika kuwa na mapungufu mbalimbali ambapo Ofisi ya TAKUKURU imeanza ufuatiliaji wa kina wa matumizi wa fedha hizo kama inavyoonekana kwenye **kiambatisho na. 1**

3.2 Uchambuzi wa Mifumo

Ofisi ilifanya jumla ya kazi **06** za Uchambuzi wa Mifumo katika sekta za **Fedha,** na **Mazingira na** kikao kimoja cha kuwekeana mikakati kuhusiana na utaratibu unaotumika katika uzoaji taka katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa iliyopo katika mifumo hiyo na kisha, kupitia vikao vya wadau, kuzishauri taasisi tafitiwa namna bora ya kuziba mianya ya rushwa iliyobainika kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho na. 2**

4. KAZI ZA UELIMISHAJI UMMA

Katika kipindi hiki, TAKUKURU Mkoa wa Mbeya iliwafikia wananchi wapatao **23,194** ambao walipata elimu ya kuzuia vitendo vya rushwa kupitia **uimarishaji wa klabu za wapinga rushwa 59** za shule za msingi na sekondari, **Semina 27, Mikutano ya hadhara 27, Makala 05, Vipindi vya redio 10** pamoja na **maonesho 08**.

5. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA TAKUKURU-RAFIKI

Vilevile katika kipindi hicho Ofisi ilitekeleza **Programu ya TAKUKURU-Rafiki** katika jumla ya Kata **7** za Mkoa wa Mbeya kwa lengo la kuongeza wigo wa ushiriki wa wadau katika mapambano dhidi ya rushwa nchini kwa kuwashirikisha wananchi kuanzia ngazi za Kata kutambua kero, kuweka mikakati ya kuzitatua, kutekeleza mikakati hiyo na hatimaye jamii kunufaika na utatuzi wa kero hizo. Jumla ya kero **09** ziliibuliwa na wananchi katika mikutano hiyo ya hadhara na kutafutiwa majawabu kutoka kwa watoa huduma kama inavyooneshwa katika kiambatisho na. 3 -

6. UCHUNGUZI NA MASHTAKA

6.1 Uchunguzi

Katika kipindi cha **Julai** hadi **Septemba, 2023** ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Mbeya ilipokea jumla ya **malalamiko 72,** ambapo kati ya hayo **44 yalihusu rushwa** na **28 hayakuhusu rushwa**. Katika malalamiko ambayo yalihusu rushwa chunguzi zilianzishwa na zipo katika hatua mbalimbali na kwa malalamiko ambayo hayakuhusu rushwa wananchi walishauriwa namna bora ya kushughulikia malalamiko yao ikiwa ni pamoja na kuwaelekeza taasisi za kupeleka malalamiko hayo.

Sekta zilizolalamikiwa zaidi katika kipindi hicho ni **Ardhi, Utawala, Fedha** na **Afya** kama inavyoonekana katika **kiambatisho na 4**

7. Mashtaka

Katika eneo la mashtaka, Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Mbeya iliendesha jumla ya **mashauri 23** katika Mahakama mbalimbali ndani ya Mkoa wa Mbeya. Katika mashauri haya, mashauri **18** ni yale yaliyokuwa yakiendelea mahakamani hadi kufikia tarehe 30/09/2023 na mashauri **5** yalikuwa ni mapya yaliyofunguliwa katika kipindi hicho. Jamhuri ilishinda mashauri 02 kati ya **03** yaliyotolewa maamuzi ndani ya kipindi hicho. Hivyo, idadi ya kesi mpaka tarehe 30/09/2023 zilizokuwa zinaendelea mahakamani zilikuwa **20**.

8. MIRADI ILIYOTEMBELEWA NA MWENGE

Katika kipindi hiki TAKUKURU (M) - Mbeya ilikagua miradi ya ujenzi 27 yenye thamani ya **Tsh 28,598,698,102.54** ambayo ilitembelewa na Mwenge wa uhuru mwaka 2023. Katika miradi hiyo miradi yote aidha ilizinduliwa au kuwekewa mawe ya msingi.

9. USHIRIKIANO NA WADAU

Katika kufikia malengo ya Taasisi kwa mujibu wa Sheria, Taasisi yetu ya TAKUKURU imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali wakati wa kutekeleza majukumu yake. Katika kutekeleza hilo TAKUKURU inashirikiana na vyombo vingine vya **Haki Jinai** ambavyo ni; POLISI, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Magereza na Mahakama.

Lengo la kuwepo kwa mashirikiano haya mahsusi ni pamoja na kuhakikisha kwamba muda unaotumika kuanzia hatua ya kufanya upelelezi mpaka hukumu inapotolewa dhidi ya raia anayetuhumiwa kwa makosa ya Jinai unakuwa ni mfupi kwa kadri inavyowezekana.

Katika kutekeleza hilo, mnamo tarehe **08/09/2023** kilifanyika kikao cha utatu kati ya kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ya Mkoa wa Mbeya, wapelelezi kutoka Ofisi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, na maafisa uchunguzi Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Mbeya Pamoja na mambo mengine yaliyojadiliwa kikao hicho kiliwatambulisha Maafisa waendesha

CamScanner

Mashtaka wa Wilaya kutoka ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoa na Mwendesha Mashtaka wa Mkoa wa Mbeya alitoa taarifa kwamba ofisi yake imeshafungua ofisi za Wilaya ambapo hapo awali hazikuwepo hivyo kila mdau wa haki jinai hususani vyombo chunguzi awatumie kuongeza ufanisi wa uchunguzi wa majalada.

Mnamo Tarehe 12/9/2023 na 15/9/2023 vilifanyika vikao kati ya Ofisi ya mashtaka Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa TAKUKURU (M) - Mbeya na Mkuu wa upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Mbeya. Lengo la vikao hivyo lilikuwa ni kukagua mahabusu za Magereza na Jeshi la Polisi.

Vilifanyika vikao viwili kati ya baadhi ya wachunguzi wa TAKUKURU (M) - Mbeya na wanasheria ofisi ya taifa ya Mashtaka ya Mkoa kuhusiana na uchunguzi wa majalada mnne ya yaliyowahusu watuhumiwa wa mtandao bandia wa kukusanya mapato wa kwa njia ya POS.

Vilevile, Ofisi ya TAKUKURU imekuwa ikiwashirikisha wananchi wa Mkoa wa Mbeya katika kuzuia rushwa kwa kubaini na kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwenye Ofisi zote za TAKUKURU zilizopo mkoani Mbeya.

Pia Ofisi imeendelea kushirikiana vizuri na waandishi wa habari katika kuhabarisha umma juu ya namna ya kuzuia na kupambana na rushwa katika utoaji na upokeaji wa huduma za jamii na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

10. MATARAJIO YETU KWA KIPINDI CHA MIEZI MITATU IJAYO

Katika kipindi cha miezi mitatu ijayo kuanzia mwezi **Oktoba** hadi **Desemba 2023,** Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Mbeya imejipanga kufanya mambo yafuatayo: -

1. Kuendelea kutekeleza Programmu ya **TAKUKURU Rafiki** kwa kufanya kwa uchache mkutano mmoja wa hadhara kila mwezi katika ngazi ya Kata kwa lengo la kuwawezesha wananchi kuibua kero ili kero hizo zilizoibuliwa ziweze kutafutiwa majawabu kutoka kwa watoa huduma.

2. Kuendelea kufanya kazi za uzuiaji rushwa kupitia uchambuzi wa mifumo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo miradi ya kitaifa hususani ya ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji inayotekelezwa mkoani Mbeya kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa iliyopo katika mifumo na miradi hiyo na kushauri namna bora ya kuiziba mianya ya rushwa iliyobainika.

3. Kuendelea kuchunguza vitendo vya rushwa na kuwafikisha watuhumiwa mahakamani baada ya kupata kibali cha Mwendesha Mashitaka, wale wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa kinyume na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na 11 ya mwaka 2007 pamoja na sheria nyingine.

11. HITIMISHO

Tunawapongeza wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwa jinsi wanavyoendelea kushirikiana na Ofisi ya TAKUKURU katika mapambano dhidi ya rushwa. Aidha, tunawasihi waendelee kushirikiana na Ofisi yetu kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kupiga **Simu ya Bure-113** au kufika katika Ofisi za TAKUKURU Mkoa na Wilaya kwa ajili ya kutoa taarifa, nasi tunaahidi kuzifanyia kazi taarifa tutakazozipokea kwa wakati na kwa usiri mkubwa.

Vilevile, tunawahasa wananchi kufuatilia na kuhoji hatua za utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyopo katika maeneo yao ili kudhibiti ubadhirifu wa fedha za miradi hiyo na tunawaalika waendelee kushiriki kwa dhati katika Programu ya **TAKUKURU-Rafiki** kwa kutambua kero zilizopo katika maeneo yao ili kero hizo zitafutiwe majawabu kutoka taasisi zinazotoa huduma kwa wananchi.

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU'.

Imetolewa na:—

Maghela P. Ndimbo,
Mkuu wa TAKUKURU (M) MBEYA.
0738150137

KIMABATISHO NA 1.
MIRADI ILIYOKUTWA NA MAPUNGUFU

NA.	MRADI WENYE MAPUNGUFU NA THAMANI YAKE	KILICHOBAINIKA	HATUA ILIYOCHUKULIWA
1	Ujenzi wa shule ya Msingi Kilambo	Fedha ya mradi imeisha na ujenzi haujakamilika.	Ufuatiliaji wa kina umeanzishwa katika mradi huu.
2	Ujenzi wa shule ya masngi Lubele	Fedha ya mradi imeisha na ujenzi haujakamilika.	Ufuatiliaji wa kina umeanzishwa katika mradi huu.
3	Ujenzi wa shule ya msingi Kasumulu	Fedha ya mradi imeisha na ujenzi haujakamilika.	Ufuatiliaji wa kina umeanzishwa katika mradi huu.

KIAMBATISHO NA 2
UCHAMBUZI WA MIFUMO.

S/N	MFUMO ULIOCHAMBULIWA	YALIYOBAINIKA	MAKUBALIANO
1.	Uchambuzi wa mfumo wa ukusanyaji na uwasilishaji wa kodi ya zuio katika ununuzi wa vifaa na huduma katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe	Kwa kipindi cha Mwaka wa fedha 2021/2022 Jumla ya **Tsh. 137, 258,376.12** kwa kipindi cha Mwaka wa fedha **2022/2023** Jumla ya fedha **Tsh. 27,198,577.37** Haikuwasilishwa katika Mamlaka ya Mapato.	TAKUKURU itafanya kikao kazi na Halmashauri, TRA Pamoja na wazabuni ili kodi hii ilipwe pia wazabuni wanaolipa kodi kwa usahihi ndio wapewe kazi katika Halmashauri hiyo
2.	Uchambuzi wa mfumo wa ukusanyaji wa kodi ya zuio katika Halmashauri ya	• Katika uchambuzi wa mfumo ilibainika kwamba kiasi cha fedha Tsh. 13,000,000/= hazijawasilishwa TRA. • Wazabuni wengi	TAKUKURU itafanya kikao kazi na Halmashauri, TRA Pamoja na wazabuni ili kodi hii ilipwe pia wazabuni wanaolipa kodi kwa usahihi ndio wapewe kazi katika

CamScanner

	Wilaya ya Chunya.	hawaoneshwi kwa wakati 'certificate inayoonesha wamekatwa kodi ya zuio.	Halmashauri hiyo.
3.	Uchambuzi wa mfumo wa ukusanyaji wa kodi ya zuio katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela.	Katika uchambuzi wa mfumo ilibainika kwamba kiasi cha fedha Tsh. 29,830,509.43 hazijawasilishwa TRA kwa mwaka 2022/2023 na mwaka 2021/2022 ni Tsh. 290,801,540.18 • Shida katika upatikanaji wa Control Number • Halmashauri hazina taarifa sahihi za kodi ya zuio.	TAKUKURU itafanya kikao kazi na Halmashauri, TRA Pamoja na wazabuni ili kodi hii ilipwe pia wazabuni wanaolipa kodi kwa usahihi ndio wapewe kazi katika Halmashauri hiyo.
4	Uchambuzi wa mfumo wa ukusanyaji wa kodi ya zuio katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali	Katika uchambuzi wa mfumo ilibainika kwamba kiasi cha fedha Tsh. 29,830,509.43 hazijawasilishwa TRA kwa mwaka 2022/2023. • Shida katika upatikanaji wa Control Number • Halmashauri kutokuwa na taarifa sahihi za kodi ya zuio	TAKUKURU itafanya kikao kazi na Halmashauri, TRA Pamoja na wazabuni ili kodi hii ilipwe pia wazabuni wanaolipa kodi kwa usahihi ndio wapewe kazi katika Halmashauri hiyo.

CamScanner

KIAMBATISHO NA 3
TAKUKURU RAFIKI

OFISI	KERO ZILIZOIBULIWA	SEKTA	HATUA ZILIZOCHUKULIWA
Mkoani	Ubovu wa Barabara za mtaa Michango mingi (mitihani, chakula n.k) katika shule za msingi.	Barabara Elimu	Kero hii iliwasilishwa kwa meneja wa TARURA (W) kwa ajili ya ufafanuzi. Afisa elimu Kata alitoa ufafanuzi kuwa wazazi wengi hawahudhurii vikao vya wazazi hivyo kutokuwa na taarifa na yaliyoafikiwa katika vikao hivyo.
Mbarali	Hapakufanyika TAKUKURU RAFIKI kutokana na maandalizi ya Uchaguzi Mdogo wa Ubunge.		
Rungwe	Kutokuwepo kwa Barabara zinazopitika katika majira yote Upungufu wa miundombinu ya maji Baadhi ya vijiji kutokuwepo kwenye miradi wa usambazaji umeme vijijini (REA)	BARABARA MAJI UMEME	TARURA (W) Rungwe imeshatengeneza baadhi ya barabara hizo na inaendelea kutengeneza nyingine kadri fedha zinavyopatikana. Mhandisi kutoka RUWASA alitoa ufafanuzi kuwa utekelezaji wa mradi bado unaendelea na ukikamilika kero ya maji itakuwa imeisha. Ofisi ya TAKUKURU itafanya ufuatiliaji kuhusiana na miradi hii na italeta mrejesho.

CamScanner

kyela	Kero ya kukatika umeme mara kwa mara	UMEME	Ulitolewa ufafanuzi kwamba inatokana na hitilafu katika mifumo ya usambazaji umeme na ratiba iliyopo kwa sasa ya upungufu wa umeme.
	Kero ya kukosekana kwa maji ya uhakika	MAJI	Mhandisi kutoka RUWASA alitoa ufafanuzi kuwa utekelezaji wa mradi bado unaendelea na ukikamilika kero ya maji itakuwa imeisha.
	Barabara kutokupitika kwa wakati wote	BARABARA	Mhandisi kutoka TARURA alitoa ufafanuzi kwamba barabara hizo zitaendelea kufanyiwa ukarabati kwa kadri bajeti inavyoruhusu, hatahivyo alitoa wito kwa wananchi kujitolea kufanya ukarabati mdogo kwa baadhi ya maeneo.
JUMLA:	**09**		

KIAMBATISHO NA 4
KESI KISEKTA

Na.	Sekta	Idadi
1	Ardhi	7
2	Ushirika	9
3	Halmashauri	6
4	Mahakama	7
5	Ujenzi	3
6	Vyama vya siasa	2
7	Elimu	5
8	Kilimo & ufugaji	4
9	Fedha	8
10	Utawala	2

CamScanner

11	Madini	1
12	Polisi	3
13	Binafsi	4
14	Maliasili na utalii	1
15	Maji	1
16	Maendeleo ya jamii	1
	Jumla:	**72**

CamScanner